**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/20.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 71 (b) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, kamati ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Jenista Joackim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) pamoja na Katibu wa Bunge na kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/20.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inaeleza kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019 katika kipindi cha hadi Machi, 2019 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi yanayojumuisha vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Bajeti ya Mwaka wa fedha 2019/2020.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/2019 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya **Sh.125,521,100,000** kati ya fedha hizo **Sh.24,441,023,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **Sh.92,764,464,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh.8,315,613,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za Maendeleo **Sh.5,000,000,000** ni fedha za ndani na **Sh.3,315,613,000** ni fedha za nje.

### 2.1 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 15, 2019 Ofisi ya Bunge ilikuwa imepokea fedha za matumizi ya kawaida kiasi

cha **Sh.73,206,843,427.00.** Kati ya fedha hizo **Sh. 58,085,266,647** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) (sawa na 63% ya bajeti yote) na **Sh. 15,121,576,780** kwa ajili ya Mishahara (PE) (sawa na 62% ya bajeti yote).

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla utolewaji wa fedha za matumizi ya kawaida (Mishahara na OC) umekuwa mzuri na umewezesha Ofisi ya Bunge na Bunge lako Tukufu kutekeleza majukumu yake vizuri.

## 2.2 Matumizi ya Fedha za Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 15 Machi 2018, Mfuko umepokea kiasi cha **Sh. 6,710,062,500** ambazo ni sawa na **asilimia 81** ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kutumika katika mwaka wa fedha 2018/19. Kati ya hizo zilizotolewa, **Sh. 4,287,500,000** ni fedha za ndani (sawa na asilimia 86 ya fedha za ndani zilizoidhinishwa) na **Sh. 2,422,562,500** ni fedha za nje (sawa na asilimia 73 ya fedha za nje zilizoidhinishwa)**.**

## 2.3 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Mfuko wa Bunge ulipanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Sh.61,000,000** ambapo hadi kufikia Mwezi Machi, 2019, Mfuko ulikuwa umekusanya kiasi cha **Sh.39,983,700 (sawa na asilimia 65.5).** Maduhuli hayo yametokana na kodi ya pango.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa Mwaka huu wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2019 Ofisi ya bunge ilitekeleza majukumu mbali mbali yaliyopangwa kama ifuatavyo:

i) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano Mitatu ya Bunge;

ii) Kuratibu na Kusimamia shughuli za Mikutano Mitatu ya Kamati za Bunge;

iii) Kuwezesha Kamati za Bunge kufanya ziara katika maeneo mbalimbali nchini;

iv) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard);

v) Kugharamia malipo ya stahili za Wabunge (Posho ya Jimbo na Usafiri);

vi) Kugharamia matibabu ya Wabunge;

vii) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa miswada;

viii) Kutoa huduma za Utafiti "Information Research" kwa Wabunge;

ix) Kuwezesha Wabunge kushiriki kwenye Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge ni Mwanachama ambayo ni SADC PF, PAP, CPA, Maziwa Makuu, IPU, ACP-EU;

x) Kuwezesha Wabunge kushiriki mashindano ya Michezo kwa Mabunge ya Jumuiya ya Afrika mashariki;

xi) Kufanya mapitio *(review)* ya Mpango Mkakati wa Ofisi kwa mwaka 2016/2017 – 2020/2021); Mpango wa Usimamizi wa Vihatarishi na kuandaa Rejesta ya Vihatarishi vya Ofisi;

xii) Kuratibu kazi ya utoaji wa habari kwa wananchi kuhusu shughuli za Kamati na Bunge;

xiii) Kuandaa vipindi vya Televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;

xiv) Kuratibu shughuli mbalimbali za utawala (ununuzi wa vifaa vya Ofisi), malipo ya maji, umeme na simu, usafi na ulinzi);

xv) Kuratibu na Kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ikiwa ni pamoja na:

a. Kufanya ukarabati na ununuzi wa vifaa ya Usalama;
b. Kufanya ukarabati wa majengo ya Ofisi za Bunge ikiwa ni pamoja na kuongeza ghorofa moja katika jengo la Utawala;
c. Ujenzi wa nyumba kwa ajili ya Makazi ya Viongozi wa Bunge – Dodoma;
d. Kusimika lifti katika jengo la Utawala na jengo la Utawala Annex;
e. Kuratibu na kusimamia mafunzo mbalimbali kwa Wabunge na Watumishi kupitia Mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge (LSP II) na Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP);

## 4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

### 4.1 Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/20

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Katika Mpango na Bajeti ya Mwaka 2019/2020 Mfuko wa Bunge umepanga kutumia kiasi cha **Sh.124,182,537,600.00** Kati ya fedha hizo **Sh.23,334,462,000.00** ni fedha za Mishahara; **Sh.93,238,564,000.00** ni fedha za Matumizi mengineyo na **Sh.7,609,511,600.00** ni fedha za Maendeleo. Kati ya fedha hizo za Maendeleo, kiasi cha **Sh.5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh.2,609,511,600.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/20 Ofisi ya Bunge inatarajia kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 54,777,000.00.**

## 4.2 Shughuli zitakazotekelezwa Katika Mwaka wa Fedha 2019/20

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/2020 Mfuko wa Bunge umepanga kutekeleza shughuli za vipaumbele kama ifuatavyo: -

a) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano Minne (4) ya Bunge;
b) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano Minne (4) ya Kamati za Bunge;
c) Kuwezesha Kamati za Bunge kufanya ziara katika maeneo mbalimbali nchini;
d) Kugharamia malipo ya stahili za Wabunge (Posho ya Jimbo na Usafiri);
e) Kugharamia matibabu ya Wabunge;
f) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard);
g) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa miswada;
h) Kutoa huduma za Utafiti “Information Research” kwa Wabunge;

i) Kuwezesha Wabunge kushiriki kwenye Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge ni Mwanachama SADC-PF, PAP, Maziwa Makuu, IPU, Mabunge ya Jumuiya ya Madola na ACP-EU;

j) Kuwezesha Mkutano wa Maspika wa Jumuiya ya Madola;

k) Kuwezesha Wabunge kushiriki mashindano ya Michezo kwa Mabunge ya Jumuiya ya Afrika mashariki;

l) Kutoa huduma ya mawasiliano ya habari kwa Wabunge kwa kuimarisha Mifumo ya Tehama na Mawasiliano kwa jamii;

m) Kuendeleza marekebisho ya mifumo ya utendaji kazi katika idara na Vitengo ili kuongeza tija na ufanisi (Mfumo wa kielektroniki wa maktaba na kutunza kumbukumbu);

n) Kuratibu na kusimamia shughuli mbalimbali za utawala (huduma kwa Wabunge, ununuzi wa vifaa vya Ofisi, malipo ya maji, umeme na simu, usafi na ulinzi) pamoja na ukarabati wa Kumbi za Mikutano na ujenzi wa Makazi ya viongozi;

o) Kuboresha utendaji kwa kutoa mafunzo mbalimbali kwa Watumishi;

p) Kuratibu na Kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ikiwa ni pamoja na:

i. Ukarabati na ununuzi wa mitambo ya usalama;
ii. Kusimika Kituo cha Matangazo ya Bunge *(Broadcasting Studio)* katika Ukumbi wa Bunge;
iii. Ujenzi wa nyumba kwa ajili ya Makazi ya Viongozi wa Bunge - Dodoma;
iv. Ukarabati wa Ukumbi wa Msekwa, Ukumbi wa Bunge pamoja na majengo ya Ofisi ya Bunge; na
v. Kuratibu na kusimamia mafunzo mbalimbali kwa Wabunge na Watumishi kupitia Mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge (LSP II) na Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP).

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

5.1 **Mheshimiwa Spika,** kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka ujenzi wa Ofisi za Wabunge katika Majimbo na kuziwekea samani ili kurahisisha utendaji kazi wao kwa kipindi wanachokuwa majimboni;

5.2 **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2018/2019 Ofisi ya Bunge inategemea kutekeleza Miradi muhimu ya maendeleo

kama vile ununuzi wa Mitambo ya Usalama, Kituo cha Matangazo ya Bunge *(Broadcasting Studio),* ukarabati wa Kumbi za Bunge pamoja na ujenzi wa nyumba za Makazi ya viongozi. Kamati ya Bunge inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha za maendeleo kwa wakati ili miradi hii ikamilike kama ilivyopangwa.

## 6.0 HITIMISHO.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

1) Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb – Mwenyekiti
2) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Makamu Mwenyekiti
3) Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
4) Mhe. Balozi Diodorus Buberwa Kamala, Mb
5) Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
6) Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
7) Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
8) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
9) Mhe. Dalali Peter Kafumu, Mb
10) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
11) Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12) Mhe. Hasna Sadi Kalunda Mwilima, Mb
13) Mhe. Dkt. Immaculate Swale Semesi, Mb
14) Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb
15) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
16) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb

17) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb

18) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb

19) Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb

20) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb

21) Mhe. Oran Manase Njeza, Mb

22) Mhe. Riziki Said Lulida, Mb

23) Mhe. Stephen Julius Masele, Mb

24) Mhe. Andrew John Chenge, Mb

25) Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb

26) Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa ushauri wa kitaalamu ambao wamekuwa wakiipa Kamati ambao umewezesha kukamilisha taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

George B. Simbachawene, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**

04 APRILI, 2019